


Ukarimu kwenye Jukwa

Na Hilary Watkins Lemon
(Imetokana na hadithi ya kweli)



Wwakati Damien alipoingia kwenye eneo la mchezo, alisikia muziki wa furaha ukichezwa. Bibi yake alikuwa amewapeleka yeye na dada yake mdogo, Adele, kuendesha jukwa yake aipendayo. Ilikuwa ni mchezo wa kuburudisha. Damien alihamasika kumwonyesha Adele jinsi ya kuucheza. Punde wakawa sambamba. Jukwa ilikuwa kubwa na yenye rangi nyingi, pamoja na farasi wadogo wengi wa kuchongwa. Watoto wenye tabasamu walikuwa juu ya farasi hao na walipunga mikono wakati wanaendesha. "Kama utamshika farasi kwenye ncha, unaweza kucheza mchezo wa mviringo!" Damien alimwambia Adele. "Unaona fimbo ambazo watoto wamezishika? Na unamwona yule mtu aliyeshika ile mviringo?" Damien alimwonyesha mfanyakazi. Mfanyakazi alikuwa amesimama karibu na ile jukwa huku ameshikilia mviringo. Walipokuwa wakiendesha juu ya jukwa, wale watoto walikuwa wakijaribu kuingiza fimbo zao kwenye mviringo ili kuichukua. Kila wakati walipochukua mviringo, mfanyakazi aliwaonyesha mwingine mpya. Adele alipiga makofi. "Ninataka kukamata mviringo yote!" alisema. Mwishowe walifika mbele ya mstari. Lakini palikuwa na farasi mmoja tu aliyebaki kwenye jukwa hiyo.

"Damien," Bibi alisema, "kwa nini tusimwache Adele achukue nafasi hii ya mwisho kwa vile yeye haja-wahi kuendesha jukwa? Wewe unaweza kuendesha zamu inayofuata?"

"Sawa," Damien alijibu kwa kunung'unika. Alimwangualia yule mfanyakazi akimsaidia Adele kupanda juu ya yule farasi wa rangi ya kahawia. Kisha mfanyakazi yule akampatia Adele fimbo ya kukamata mviringo.

Muziki ukaanza, na ile jukwa ikaanza kuzunguka. Damien alimwangualia Adele kutoka upande ule pamoja na Bibi. Lakini Adele alishikilia ile fimbo kwa nyuma! Badala ya kushikilia fimbo kwenye mshikio mkubwa, yeye alishika mwisho mrefu, mwembamba unaotumika kudaka mviringo.

"Adele, geuza fimbo yako!" alipiga kelele. Lakini Adele alionekana kutomsikia kutokana na kelele. Wakati anaupita mviringo, fimbo yake ikaugusa. Lakini mshikio ulikuwa mkubwa sana kuweza kuingia ndani ya mviringo.

"Adele, fimbo yako!" Damien alijaribu tena. "Wewe hutaweza kukamata mviringo kama unashika fimbo namna hiyo!"

Lakini Adele hakumsikia? Yeye alitabasamu na kucheka wakati jukwa ilipokuwa inazunguka. Fimbo yake iligusa mviringo tena na tena. Hakukamata hata mviringo mmoja.

Damien aliguna. Adele alikuwa anapoteza zamu yake! Kama yeye angekuwa kwenye jukwa, angekamata mviringo yote.

Mzunguko ulivyoisha, alimkimbilia Adele.

"Nilikwambia namna ya kushika hii fimbo!" alisema kwa sauti. "Kwa nini hukunisikiliza mimi? Ulifanya makosa!"

Adele hakumpigia makelele Damien. Hakulia. Yeye alisimama tuli na alionekana mdogo, mdogo, mdogo.

Moyo wa Damien ulidunda kwa nguvu, na uso ukawa mwekundu. Ilimfanya akasirike kumwangualia Adele akiikosa mviringo ile yote. Lakini ilikuwa ni mara yake ya kwanza tu. Hata hivyo, ilionekana kwamba alifurahia mchezo hadi sasa.

Damien alijihisi vibaya sana. Damien alitamani

asingemfokea dada yake.

"Samahani," alisema kwa upole. "Sijakufanyia vizuri."

Adele alitazama juu.

"Unaonaje kama mimi ningekupatia baadhi ya vidokezo kuhusu kukamata mviringo?" Damien alisema. "Mimi nitakaa nyuma yako kwenye jukwa na nitakusaidia."

Adele aliitikia kwa kutikisa kichwa.

Kisha Damien akamgeukia Bibi. "Tunaweza kupata tiketi mbili ili Adele aweze kujaribu tena?"

Bibi alitabasamu. "Bila shaka!" ●

Hadithi hii ilitokea huko Ufaransa.

